الأخلاق في الإسلام - سواحيلي

# TABIA KWENYE UISLAMU



جمعية الدعوة بالزلفي

جمعية الدعوة والإرشاد وتوعية الجاليات بالزلفي
هاتف: ٠١٦ ٤٢٣٤٤٦٦ ـ فاكس: ٠١٦ ٤٢٣٤٤٧٧

# TABIA KWENYE UISLAMU

## الأخلاق في الإسلام - سواحيلي

Kimetasiriwa na kuhakikiwa na:
Abubakar Kassimu Abubakar
Ally Nassoro Ally
Abdallah Ally Chumbe

جمعية الدعوة والإرشاد وتوعية الجاليات في الزلفي
هاتف: 164234466 966 ـ فاكس: 164234477 966

# الأخلاق في الإسلام - سواحيلي

**أعده وترجمه للغة السواحيلية**

**جمعية الدعوة والإرشاد وتوعية الجاليات بالزلفي**

**الطبعة الأولى: ١٤٤٤/٠٦ هـ**

ⓒجمعية الدعوة والإرشاد وتوعية الجاليات بالزلفي ، ١٤٤٤هـ

***فهرسة مكتبة الملك فهد الوطنية أثناء النشر***

جمعية الدعوة والإرشاد وتوعية الجاليات بالزلفي
الأخلاق في الإسلام / لغة السواحلية. / جمعية الدعوة والإرشاد وتوعية الجاليات بالزلفي .- الزلفي ، ١٤٤٤هـ

٣٦ ص ؛ ..سم

ردمك: ٩-١٤-٨٣٩٩-٦٠٣-٩٧٨

١- الاخلاق الاسلامية ٢- الاداب الاسلامية أ.العنوان

ديوي ٢١٢,١ ١٤٤٤/٥٨٢٧

**رقم الإيداع: ١٤٤٤/٥٨٢٧**

**ردمك: ٩-١٤-٨٣٩٩-٦٠٣-٩٧٨**

بسم الله الرحمن الرحيم

# UTANGULIZI

Sifa njema zote ni zake Allah, Na Rehema na Amani ziwe juu yake Mjumbe wa Allah. Ama baadha ya hayo:

Tunamshukuru Allah -mtukufu- kwa kutuneemesha neema ya Uislamu, na akatuimiza sana kushikamana na tabia njema, na akaweka malipo makubwa juu yake.

Tabia njema ni sifa miongoni mwa sifa za Manabii na waja Wema. Kwa kuwa zinapelekea kupandishwa mtu daraja. Na hakika Allah -Mtukufu- amemsifu Mtume wake Muhammad kupitia ayah ambayo imekusanya tabia njema zote, amesema -Mtukufu: "**Na hakika wewe upo juu kwa tabia njema**)" [Al-qalam: 4].

Na tabia njema huleta upendo na mshikamano. Na tabia mbaya huzalisha kuchukiana na kuhusudiana. Na athari za mwenye tabia nzuri zipo wazi katika Dunia na Akhera, na Allah amemkusanyia kati ya Taqwa (Ucha mungu) na Tabia nzuri, amesema

Mjumbe wa Allah -Rehma na Amani za Allah ziwe juu yake-: “**Mengi ambayo yatawaingiza watu peponi ni kumcha Allah na kuwa na Tabia njema**” [ameipokea Tirmidhi na Haakim].

Na tabia njema: Ni kuwa na uso wa bashasha, kutenda mazuri na kuto waudhi watu. Haya Pamoja na maneno mazuri anayojilazimisha Muislamu, kuidhibiti na kuificha hasira yake, na kuvumilia maudhi. Na amesema Mjumbe wa Allah -Rehema na Amani za Allah ziwe juu yake-: **“Nimetumwa kwa ajili ya kukamilisha Tabia njema”** [ameipokea Ahmadi, Al-baihaqey na Al-haakim na ameisahihisha].

Na Nabii -Rehema na Amani za Allah ziwe juu yake- alimuusia Abu Hurairah -Allah amridhie-: “**Ewe Abu Hurayrah! Jilazimu na tabia njema**” Abu Hurayrah akasema: Tabia njema ni zipi ewe mjumbe wa Allah? Akasema: “**Ni kumuunga ndugu yako aliekukata, kumsamehe alie kudhulumu na kumpa aliekunyima”** [ameipokea Al-bayhaqy kitabu chake Shuab].

Angalia ndugu yangu Muislamu hii athari kubwa na thawabu nyingi za hii sifa tukufu, amesema Mjumbe

wa Allah -Rehema na Amani za Allah ziwe juu yake-: "**Hakika Mtu hufikia daraja la Mfungaji mwenye kusimama usiku kutokana na Tabia yake njema**" [ameipokea Ahmad], na ameifanya -Rehema na Amani za Allah ziwe juu yake- Tabia njema kuwa ni miongoni mwa ukamilifu wa Imani ya mtu, Akasema: "**Mkamilifu wa Imani kwa waumini ni yule mzuri wao kitabia".**

Na zingatia ndugu yangu kauli ya Mjumbe wa Allah -Rehema na Amani za Allah ziwe juu yake- "Mtu Anaependeza Zaidi kwa Allah ni yule ambae anawanufaisha watu, na matendo yanayopendeza Zaidi kwa Allah -mtukufu- ni furaha ambayo utaingiza kwa ndugu yako Muislamu, au ukamtatulia tatizo, au ukamlipia deni, au ukamuondolea njaa, na Kwenda kumsaidia ndugu yangu muislamu katika shida, inapendeza zaidi kwangu kulikoni kujilazimisha kukaa msikitini kufanya ibada mwezi mzima" [Ameipokea Twabarany].

Ndugu yangu Muislamu…Neno laini jema ulisemalo unapata malipo mema, na inakuwa ni sadaka yako, amesema Mjumbe wa Allah -Rehema na Amani za Allah ziwe juu yake- "**Na neno jema ni sadaka**" [wameafikiana Bukhary na Muslim kuwa ni sahihi]. Na yote

hayo ni kwa sababu neno jema lina athari nzuri, kwani mioyo huwa karibu, Nafsi hupendana, huondoa kutengana.

Na maelekezo ya kiutume katika kuhimiza Tabia njema na kuvumilia maudhi ni mengi, miongoni mwa hayo ni: Kauli yake -Rehema na Amani za Allah ziwe juu yake- “Muogope Allah popote uwapo, na fatilia ovu ulilolitenda kwa kutenda jema italifuta ovu hilo, na uamiliane na watu kwa tabia njema” [Ameipokea Altirmidhy].

Na tabia njema ni lazima kwa Muislamu kila sehemu na wakati wowote, hilo humpendezesha kwa watu, humuweka karibu nao kwa kila njia anayoipita, na kila sehemu anayo kwenda, Na hata tonge analolinyanyua kumlisha mkewe hulipwa kwa kufanya hivyo katika Uislamu, Amesema -Rehema na Amani za Allah ziwe juu yake-: “Na hakika chochote unachokitoa katika matumizi ni sadaka, mpaka tonge ulilolinyanyua kwenye kinywa cha mke wako (ni sadaka)” [Ameipokea Bukhary].

Ndugu yangu kipenzi!...Waumini ni Ndugu, inapasa kwa Muislamu kumpendelea ndugu yake anacho kipendelea kwa nafsi yake… Angali kile

unachoipendelea nafsi yako umfanyie ndugu yako, na kile unachokichukia basi kiweke mbali nae. Jihadhari kumpuuza yule mwenye kumuamini Allah kuwa ni mlezi, na Uislamu ndio Dini, na Muhammad -Rehema na Amani za Allah ziwe juu yake- ni Mtume na ni Nabii, Hakika hilo amelitahadharisha kwa kusema: "**Yatosha mtu kuwa ni mtu wa shari kwa kumdharau ndugu yake Muislamu**" **[Ameipokea Muslim].**

Ndugu yangu Muislam! Njia ni rahisi na Ibada ni nyepesi nyakati zote. Amesema Mjumbe wa Allah -Rehema na Amani za Allah ziwe juu yake- kumuambia Abu Dardaai: "Hivi nikujuze juu ya Ibada zilizo nyepesi na rahisi zaidi kwa Mwili kiutendaji" akasema Abu Dardaai: Niambie ewe Mjumbe wa Allah! Akasema -Rehema na Amani za Allah ziwe juu yake- "**Jilazimishe kunyamaza na tabia nzuri. Kwani hakika hautafanya chengine mfano wake**".

**N**a malipo ya tabia njema kwa Muumini yanalingana na malipo ya ambae anasimama usiku mzima na anafunga mchana. Kwa hiyo Muumini kama anavyosema mjumbe wa Allah -Rehema na Amani za Allah ziwe juu yake- "**Atafika daraja la**

**Mfungaji mwenye kusimama kiswali usiku kutokana na Tabia yake njema"** Na kwa mazingatio haya alikuwa Swahaba mtukufu Abu Dardaai akisema: "Hakika mja Muislamu anakuwa na tabia zake njema mpa tabia zake njema zinamuingiza peponi, na anafanya tabia mbaya mpaka tabia zake mbaya zinamuingiza motoni".

## ALAMA ZA TABIA NZURI

Hakika zimekusanyika alama za tabia nzuri kwenye sifa nyingi, miongoni mwa hizo ni:

Mwanadamu kuwa na haya nyingi, asiekuwa na maudhi, mwingi wa wema, msema kweli, mchache wa maneno, mwingi wa matendo, sio mwenye porojo, mwema mwenye kuunga udugu, mwenyesubra Zaidi, mwenye kushukuru, mwenye kuridhia, Mtulivu, Mpole, msafi, mwenye kupenda kheri, sio mwenye kulani wala kutusi, wala kufitini na kusengenya, wala hana haraka na mifundo, na wala sio bahili wala asidi, mwenye bashasha nyingi, anapenda na kuridhia kwa ajili ya Allah na anachukia kwa ajili ya yake.

Na mtu mwenye tabia nzuri anavumilia maudhi, na siku zote huwapa udhuru watu kutokana na makosa wanayoyafanya, na anafanya kila njia ya kujiepusha kufatilia makosa yao na kutafuta aibu zao, Muumini haiwezekana kuwa na hali yeyote ile katika hali za tabia mbaya.

Na Nabii kwenye sehemu nyingi katika mafundisho yake anaisistiza umuhimu wa tabia njema, na malipo makubwa ambayo anayapata mwenye kusifiwa kwa tabia nzuri.

Kutoka kwa Osama bin Sharik amesema: "Tulikuwa tumekaa na Mjumbe wa Allah -Rehema na Amani za Allah ziwe juu yake-... wakamjia Watu wakasema: "Ni nani anaependeza Zaidi kwa Allah -mtukufu- katika waja wa Allah? Akasema: "Ni yule mzuri wao kitabia" [ameipokea Twabaraniy].

Na kutoka kwa Abdi-llahi bin Omar – Allah awaridhie yeye na baba yake- amesema: nimemsikia Mjumbe wa Allah -Reheme na Amani za Allah ziwe juu yake- akisema: "Je niwaambie aliekuwa kipenzi wangu zaidi kati yenu, na atakaekuwa karibu yangu Zaidi kati yenu kimakazi siku ya kiyama?" wakasema ndio tuambie

ewe Mjumbe wa Allah. Akasema: “Ni yule mzuri wenu kitabia” [ameipokea Ahmad].

Na akasema -Rehema na Amani za Allah ziwe juu yake-: “**Na hakuna kitu Kizito Zaidi katika mzani wa mja siku ya kiyama kishindacho tabia nzuri…**” [Ameipokea Ahmad].

## TABIA ZA MTUME -Rehema na Amani za Allah ziwe juu yake-:

Hakika alikuwa Mjumbe wa Allah -Rehema na Amani za Allah ziwe juu yake- mfano wa hali ya juu kwenye zile tabia anazowalingania maswahaba zake, na alikuwa anapandikiza tabia bora kwa maswahaba zake kutokana na mwenendo wake, kabla hajapandikiza tabia hizo kupitia maneneo yake ya hikma na mawaidha.

Kutoka kwa Anas -Allah amridhie- amesema: "Nimemtumikia Mjumbe -Rehema na Amani za Allah ziwe juu yake- miaka kumi, ninaapa kwa Allah hajaniambia nyamaza kabisa, wala hajaniambia kwa kitu ambacho nimekifanya kwanini umekifanya hiki? Na kwanini usinge fanya hivi?” [ameipokea Muslim]. Na kutoka kwa yeye Anasi -

Rehema na Amani za Allah ziwe juu yake- amesema: “Siku nilikuwa ninatembea Pamoja na Mtume wa Allah -Rehema na Amani za Allah ziwe juu yake- mtume akiwa amevaa Joho nzito, akakutana na Mwarabu akamvuta kwa nguvu adi nikaona shingo ya Mtume wa Allah, ikiwa imeathiriwa na upande wa ile nguo kutokana na kuvutwa kwa nguvu, kisha akasema: Ewe Muhammad toa amri nipewe katika mali ya Allah uliyonayo!, Mtume wa Allah akamgeukia yule Mwarabu na akacheka na kuidhinisha apewe mali” [Ameipokea Bukhary na Muslim].

Na aliulizwa Aisha -Mke wa Nabii -Rehema na Amani za Allah ziwe juu yake-: mambo aliyokuwa akiyafanya Mtume nyumbani kwake? Akasema mama Aisha: “Alikuwa akiihudumia familia yake na unapofika muda wa Swala anatawadha na anatoka Kwenda kuswali” [ameipokea Muslam].

Na kutoka kwa Abdillahi bin Haarith amesema: Sijawahi kuona yeyote mwenye tabasamu nyingi kama alivyokuwa Mtume wa Allah -Rehema na Amani za Allah ziwe juu yake-! [Ameipokea Tirmidhy]. Na Tabia bora zenye kujilikana kwa Mtume - Rehema na Amani za Allah ziwe juu yake- nikuwa

mkarimu wala si bakhili wa kitu chochote kile, ni shujaa ambae harudi nyuma kupingana na haki hata siku moja, nimuadilifu hafanyi ubaya kwenye hukumu kabisa, mkweli na muaminifu kwenye Maisha yake tote.

Kutoka kwa Jaabir -Allah amridhie- amesema: Hajawahi kuombwa Nabii -Rehema na Amani za Allah ziwe juu yake- chochote na akasema: Sitaki" [wameafikiana Bukhary na Muslim]. Mtume alikuwa akitaniana na maswaaba zake, kuchanganyikanao, kucheza na Watoto wao, kukaanao karibu sana, kujibu wito, kuwatembelea wagonjwa na anakubali msamaha kwa mwenye kuutaka.

Na alikuwa akiwaita Maswaaba zake kwa majina mazuri wanayoyapenda na wala hakatishi mazungumzo ya yeyote kati yao. Kutoka kwa Qatada amesema: Kipindi ulipokuja ujumbe wa Najashi alisimama Nabii -Rehema na Amani za Allah ziwe juu yake- akiwahudumia, Maswaaba wake wakamwambia: Sisi tunatosheleza, Mtume akasema: Hakika hawa waliwakarimu jamaa zetu, na ninapenda niwafanyie hivyo. Na akasema: Hakika mimi ni mja ninaekula, kukaa kama mja waja

wengine, na alikuwa akipanda Punda, kuwatembelea maskini na kukaa na mafukara.

## UKWELI:

Hakika Muislamu mkweli yupo kwa Mola wake mlezi, mkweli kwa watu wote, na ni mkweli katika hali zake zote, ni mkweli kwenye maneno yake na ni mkweli kwa vitendo vyake. Anasema Allah Mtukufu: "**Enyi mlioamini muogopeni Mola wenu na kuweni Pamoja na wakweli**" [Al-taubah: 119].

Na kutoka kwa Aisha -Allah amridhie- amesema: "Hakuna tabia iliyochukiza zaidi kwa Mtume -Rehema na Amani za Allah ziwe juu yake- kama vile uongo…" [Ameipokea Ahmad].

Na aliulizwa Mjumbe wa Allah -Rehema na Amani za Allah ziwe juu yake: "Hivi Muumini anaweza kuwa Dhalimu (mwenye kudhulumu)? Akasema: Ndio! Akaambiwa: Muumini anaweza kuwa Bahili? Akasema: Ndio! Akaambiwa: je Muumini anaweza kuwa muongo? Akasema: Hapana…." [Ameipokea Maliki].

Na uongo kwenye Dini ni miongoni mwa machukizo mabaya sana na ndio uongo mkubwa Zaidi, na malipo

yake ni moto, kwa kauli yake -Rehema na Amani za Allah ziwe juu yake: “Yeyote mwenye kunizulia uongo (kwenye dini) kwa kukusudia, basi ajiandalie makazi yake ni motoni” [Ameipokea Bukhary].

Dini yetu ya Uislamu inatuhimiza juu ya kupandikiza tabia ya ukweli kwenye nafsi za Watoto ili wakuwe nayo: Kutoka kwa Abu Hurayra -Allah amridhie- kutoka kwa Mtume -Rehema na Amani za Allah ziwe juu yake- Amesema: “Mwenye kumwambia mtoto njoo uchukue hiki, kisha asimpe huo utakuwa ni uongo” [Ameipokea Ahmad].

Na hakika Mtume -Rehema na Amani za Allah ziwe juu yake- amehimiza umma wake kujiepusha na uongo hata ukiwa ni kwa njia ya utani, na ameahidi kupata nyumba kati kati ya pepo kwa yule ambabe atajiepusha na uongo japo ni njia ya utani, amesema -Rehema na Amani za Allah ziwe juu yake-: “Mimi ni mdhamini wa nyumba kati kati ya Pepo kwa yule ambae ataacha uongo japo ikiwa ni jambo la utani” [Amaipokea Abuu Daudi].

Mfanyabiashara huenda akasema uongo pale anapotangaza bidhaa yake, Na Mtume -Rehema na Amani za Allah ziwe juu yake- ametahadharisha

hivyo, kwa kusema: “Haiwi halali kwa Muislamu anauza bidhaa huku anajua kosoro ya bidhaa hiyo, isipokuwa inapasa kumueleza -mnunuzi- kasoro hiyo” [Ameipokea Bukhary].

## UAMINIFU:

Uislamu unawaamrisha wafuasi wake kutekeleza na kutunza Amana mbali mbali, na Mtu amchunge Mola wake kwa kila alifanyalo liwe dogo au kubwa. Muisalamu ni muaminifu kwenye kuyatekeleza aliyowajibishwa na Allah, na ni muaminifu katika kuamiliana na watu, Na uaminifu ni Mtu kujihimu (kupupia) kuifanya kazi aliyokalifishwa kwa ukamilifu mzuri.

Anasema Allah -mtukufu-: “**Hakika ya Allah anawaamrisheni mzirudishe (kutimiza) Amana kwa wenyewe, na mnapo hukumu baina ya watu muhukumu kwa uadilifu”** [Al-nisaa: 58].

Na amessema Mtume -Rehema na Amani za Allah ziwe juu yake-: “**Hawi na Imani (kamilifu) yule ambae hana uaminifu**” [Amaeipokea Ahmad]. Na Uaminifu haukuwa kama wanavyoufahamu baadhi ya watu kuwa ni kuhifadhi kitu ulichowekewa,

isipokuwa Uaminifu una maana pana Zaidi ya hiyo. Na kutekeleza Uaminifu ni Mtu kuwa ni mwenye kufanya vizuri kazi yeyote ambayo amekabidhiwa, au wajibu, sawa uwe ni wa kidini au Kidunia.

## UNYEYEKEVU:

Muislamu ananyenyekea pasi na kujidhalilisha, na wala haitakikani kabisa Muislamu kuwa na kiburi, Anasema Allah -Mtukufu-: "**Na wafanyie upole wale wanaokufata mioni mwa Waislamu"** [Al-shuaraa: 215].

Na Mtume -Rehema na Amani za Allah ziwe juu yake- anasema: "**Hakuwahi yeyote kunyenyekea kwa Ajili ya Allah isipokuwa alipandishwa daraja"** [Ameipokea Muslim].

Na amesema -Rehema na Amani za Allah ziwe juu yake-: "**Hakika Allah ameniteremshia wahyi (ufunuo) kuwa kuweni wanyenyekevu mpaka asijifaharishe yeyote yule kwa mwenzake na wala asimdhulumu yeyote Yule mwenzake**" [Ameipokea Muslim].

Na miongoni mwa Ishara za kunyenyekea ni: Kukaa na Mafukara na Masikini, na kutojikweza mbele yao, kuwa na bashasha na watu, na wala asijione

kuwa yeye ni mtu bora kuliko mwengine, na hakika alikuwa Mtume -Rehena na Amani za Allah ziwe juu yake- Akifagia nyumba yake na yeye ni Nabii wa Umma huu, na akikamua Mbuzi, akifua nguo, akila Pamoja na mtumishi wake, akinunua bidhaa sokono na kuwapa mikono Waislamu mdogo na mkubwa, Tajiri na masikini.

## HAYA:

Hakika kuwa na Haya ni jambo katika mambo ya kiimani, na Haya huleta kheri kama alivyosema Mtume -Rehema na Amani za Allah ziwe juu yake- kupitia mapokezi ya Bukhary na Muslim, Na kiigizo cha Muislamu katika hizi tabia njema ni Mtume wa Allah -Rehema na Amani za Allah ziwe juu yake- kwa kuwa alikuwa ni mwingi wa Haya, Na kutoka kwa **Abii Saidi** amesema: "…Pindi Mtume anapoona kitu ambacho anakichukia tunamjua kupitia uso wake" [Amepokea Bukhary].

Na kuwa na Haya kwa Muislamu hakumzuii kuisema Haki, au kutafuta Elimu, au kuamrisha mema, au kukataza mabaya.

Haya haikumzuia Ummu Sulaymu kusema: Ewe mjumbe wa Allah, hakika Allah haoni haya katika Haki, je mwanamke anapo ota anawajibika kuoga? Akasema: “Ndio pale anapoona maji (manii)” [Ameipokea Bukhary].

Lakini Haya inamzulia Muislam kufanya matendo mabaya, au kuwa na mapungufu kwenye kazi alizokalifishwa, au kuweka wazi siri za watu na kuwafanyia ubaya.

Na kuona Haya mbele ya Allah ni bora Zaidi, Muislamu anatakiwa aone Haya mbele ya Muunba wake ambae amemleta Duniani na Akamneemesha, Aone Haya kuwa na mapungufu kwenye kumtii Allah, au katika kumshukuru kutokana na Neema zake, Amesema -Rehema na Amani za Allah ziwe juu yake-: “Allah ndio mwenye haki Zaidi kuona Haya (mbele yake) kuliko Watu” [Amaipokea Bukhary].

# TABIA MBAYA:

## Dhuluma:

Hakika Muislamu wa kweli hamdhulumu yoyote, kwa kuwa Uislamu umeharamisha kudhulumu, amesema Allah -Mtukufu-:'' na mwenye kudhulumu miongoni mwenu tutamuonjesha adhabu kubwa'' [Al-Furqan 19].

Na imekuja katika Hadithi Al-Qudsi (takatifu) maneno yake Allah mtukufu: "Enyi waja wangu nimeiharamishia nafsi yangu kudhulumu, na nikaifanya Dhuluma kuwa ni haramu kwenu nyinyi basi msidhulumu" [Ameipokea Muslimu].

**Na Dhuluma zipo aina tatu, nazo ni**:

1- **Mja kumdhulumu Mola wake**, na inakuwa ni kwa kumkanusha Allah -Mtukufu-, Amesema -alietakasika na mapungufu -: "**Na makafiri (waliokanusha) hao ndio wenye kudhulumu**" [Al-baqara: 254]. Na inakuwa ni kwa kumshirikisha Allah kwenye Ibada, nako ni kuzielekeza baadhi ya Ibada kwa asiye kuwa Allah, amesema Allah -Mtukufu-: "**Hakika ushirikina ni Dhuluma kubwa"** [Luqmaan: 13].

2- Mja kumdhulumu mja mwenziwe: Na huwa kwa kuwaudhi kwenye heshima zao, au miili yao, au mali zao pasi na haki yeyote, amesema -Rehema na Amani za Allah ziwe juu yake-: "Muislamu yeyote ni haramu kwa Muislamu mwenzie: Damu yake, Mali yake na Heshima yake" [Ameipokea Bukhary].

Na amesema -Rehema na Amani za Allah ziwe juu yake-: "Yeyote ambae ana chochote cha dhulma cha ndugu yake Muislamu, ikiwa ni kumvunjia heshima au kitu chochote, basi arudishe leo leo -kabla haijafika siku- ambayo hakutakuwa na Dinari wala Dirhamu, itakapokuwa ana jema litachukuliwa kiasi cha alivyomdhulumu, na endapo hana mema aliyoyatenda, hapo yatachukuliwa mabaya ya aliemdhulumu na kubebeshwa yeye" [Ameipokea Bukhary].

3- Mtu kuidhulumu Nafsi yake: nako ni kwa kuyatenda yaliyoharamishwa, amesema -Mtukufu-: "**Na wala hawakutudhulumu lakini walikuwa wamezidhulumu Nafsi zao**" [Al-baqarah:57]. Kwa hivyo kuyafanya

yaliyoharamishwa ni kuidhulumu Nafsi, kwani kufanya hivyo kunawajibisha kupata Adhabu kutoka kwa Allah.

## Husda:

Husda ni miongoni mwa tabia mbaya ambazo Muislamu anapaswa kutokuwa nazo kabisa, kwa sababu ndani ya Husda kuna upingaji wa ugavi wa Allah kwa waja wake, Amesema Allah: “Au wanawafanyia Hasadi watu kutokana na yele ambayo amewapa Allah katika fadhila zake” [Al-nisaa: 54].

Na Husda zipo aina mbili:

a- Ni mtu kutamani kuondoka kwa Neema aliyo nayo mwengine kama vile Mali, au Elimu, au cheo ili azipate yeye.

b- Ni Mtu kutamani Neema za mwenzie ziondoke hata ikiwa yeye hatozipata.

Anasema Mtume -Rehema na Amani za Allah ziwe juu yake-: “Thadharini na Husda, hakika Husda inakula matendo mema kama vile Moto unavyokula (kuteketeza) Kuni au Majani” [Ameipokea Abuu Daudi].

Na wala si katika Husda kutamani kupata Neema mfano wa alizo nazo mwengine pasi na kutamani zimuondokee.

## Kughushi (kufanya Hadaa):

Muislamu ni mwenye kuwafanyia wema ndugu zake, hamfanyii Hadaa yeyote, bali hupendelea kwa ndugu zake kile akipendacho kwa nafsi yake, Anasema Mtume -Rehema na Amani za Allah ziwe juu yake-: "Yeyote mwenye kutufanyia ghishi (Hadaa) basi huyo si miongoni mwetu" [Muslimu].

Na katika mapokezi mengini anayoyapokea Imam Muslimu kwamba Hakika Mtume wa Allah -Rehema na Amani za Allah ziwe juu yake- alipita kwenye Rundo la chakula, akaingiza mkono wake, akapatwa na unyeunyevu mkononi mwake, akasema: "Ewe Muuzaji chakula ni nini hii?" akasema: kimenyeshewa na Mvua ewe Mtume wa Allah, akasema: "Kwa nini usiweke juu ya chakula ili watu waone! Yeyote mwenye kufanya Hadaa (kughushi) si katika sisi".

## Kughurika (kujiona):

Huenda akaghurika Mwanadamu kwa sababu ya elimu yake, Na ikamfanya ajikweze na kuwadharau wengine, au hata wanzuoni.

Huenda mwanadamu akaghurika kwa mali zake, akajikweza kwa watu kwa sababu hiyo.

Huenda akadanganywa na nguvu zake, au kwa ibada zake na mfano wa hayo.

Lakini Muislamu wa kweli anajiepunsha na kujiona na kujitahadhari nao, na anakumbuka kwamba hakuna lililomtoa Iblisi peponi ispoluwa ni kujiona kwake, na hilo ni pale Allah alipomuamrisha kumsujudia Adamu, akasema: Mimi ni bora kuliko yeye, kwa kuwa umeniumba kwa moto na umemuumba yeye kwa udongo, na ikawa hii ndio sababu ya kutolewa kwenye Rehema za Allah.

Na jinsi ya kuitibu tabia hii ni Mtu kujua hakika zile neema alizopewa na Allah leo, ikiwa ni Elimu, au Mali, au Afya njema, na mfano hivyo, hakika ya Allah anaweza kuviondoa Muda wowote.

# MIONGONI MWA MBINU ZA KUPATA TABIA NJEMA:

Hakuna shaka kuwa jambo zito kwenye maumbile ya kibinadamu ni kubadilisha tabia ambazo nafsi imeumbwa nazo, lakini hili si kuwa linashindikana wala haliwezekani, isipokuwa kuna sababu nyingi, na mbinu mbali mbali, na kwa kuzifuata mbinu hizo mwanadamu anaweza kupata tabia nzuri, miongoni mwa mbinu hizo ni:

## Kusalimika kwa Itikadi:

Na Itikadi ni jambo kubwa sana, kwani Tabia -kwa kawaida yake- ni matunda ya kile ambacho anakibeba mwanadamu kifikra, Itikadi anayoitakidi na yale anayoyatekeleza kwenye Dini.

Kisha Itikadi ndio Imani, na ukamilifu wa Imani kwa waumini ni yule mzuri wao zaidi kitabia, endapo itikadi itakuwa sahihi basi Tabia zinakuwa nzuri kwa kufuata Itikadi, kwani Itikadi sahihi inampelekea mwenye itikadi hiyo kuwa na tabia njema, kama vile ukweli, ukarimu, upole, ushujaa na mfano wa hayo. Kama pia itikadi hiyo inavyomzuia

na tabia mbaya kama vile uongo, kupenda mali, ubahili, ujinga na mfano wa hayo.

## Dua:

Dua ni mlango mkubwa, na pindi unapofunguliwa kwa mja zinafululiza kwake kheri nyingi na kuvuna baraka tele.

Na yeyote ataetaka kujipamba kwa tabia njema na kujiepusha na tabia mbaya, basi ajiegemeze kwa Mola wake ili ampe tabia njema na kumuondolea tabia mbaya, Dua ina faida kwenye hili na mengineyo, na kwa hili alikuwa Mtume -Rehema na Amani za Allah ziwe juu yake- myenyekezu zaidi akimuomba amruzuku tabia nzuri, na alikuwa akisema kwenye Dua yake ya ufunguzi wa Swala: “Ewe Allah niongoze kuwa na Tabia nzuri, hakuna muogozaji wa uzuri wake isipokuwa ni wewe, na uniondolee ubaya wake na hakuna muondoaji wa ubaya wake isipokuwa ni wewe” [Muslimu].

## Kupambana (na nafsi):

kupambana na nafsi au kujipinda kunafaa sana kwenye suala hili, hakika yule ambae atailazimisha nafsi yake kushikamana na mambo mazuri, na akailazimisha kujiepusha na mabaya kwa hilo atapata kheri nyingi, na kumlinda na shari

iliyompata, Na Tabia kuna ambazo hutokana na kimaumbile, na nyengin hupatiakana kwa mafunzo na kuzitenda.
Na kujipinda haina maana ya mtu kuilazimisha nafsi yake mara moja, au mbili, au Zaidi, isipokuwa maana yake kuilazimisha nafsi yake mpaka unamkuta umauti, na kwa hili hakika kujipinda ni Ibada na Allah **-**Mtukufu- anasema: "**Muabudu Mola wako mpaka ukujie umauti"** [AL-hijri: 99].

## Kujihisabia (kujitathmini):

hii ni kuikosoa Nafsi pale inapofanya tabia mbaya na kuifanya isiweze kurudia kufanya tabia hizo mara nyingine.

## Kuzingatia matokeo mazuri ya tabia njema:

kwani hakika kujua matunda ya vitu, na kufikiri kiundani uzuri wa mwisho wake, ni sababu kubwa inayosukuma kulifanya, na kujifananisha nalo na kujitahidi kuifanya.

## Kufikiria mwisho mbaya wa tabia mbaya:

Nako nikuzingatia yanayoletwa na Tabia mbaya, miongoni wa majuto yenye kudumu, na huzuni anayodumu nayo, na hasara na majuto na kuingiza chuki kwenye mioyo ya wanadamu.

## Kujihadhari na kukata tamaa kwa kutotengamaa Nafsi:

Kukata tamaa si jambo zuri kwa Muislamu na wala halilingani nae siku zote, isipokuwa anatakiwa kuyapa nguvu matakwa yake, kujitahidi kuikamilisha nafsi yake na kujipinda kuepuka kasoro zake.

## Kujilazimisha kuwa na Bashasha na tabasamu na kujiepusha kukunja uso:

Hakika Mtu kutabasamu mbele ya uso wa ndugu yake Muislamu ni sadaka inayolipwa. Kama alivyosema Nabii -Rehema na Amani ziwe juu yake-: "Kufurahi kwako mbele ya uso wa ndugu yako ni Sadaka" [Ameitoa Tirmidhy].

Na akasema -Rehema na Amani za Allah ziwe juu yake-: "Msipuuzie chochote katika mambo mema,

japo kuwa kumuonyesha ndugu yako Muislamu Uso wenye bashasha” [Ameipokea Muslim].

**Kusamehe na kujisahaulisha** ni miongoni mwa Tabia za wakubwa na watukufu, na sifa hizi mbili ni miongoni mwa sifa zinazobakisha, na kukinga dhidi ya uadui.

## Upole:

Upole ni miongoni mwa tabia tukufu, na inapasa kuwa na tabia hii kwa wenye akili. Nayo ni kuidhibiti Nafsi pale inapopata yenye kuikasirisha. Na wala haina maana kwamba kutokasirika ndio sharti la Upole, Isipokuwa mtu pale anapo pata yale ambayo ni yenye kukasirisha anajizuia kwa sababu ya upole wake. Na Mtu anapokuwa na sifa ya upole anapendwa na wengi, wanakuwa wachache wabaya wake na hupandishwa daraja.

## Kupingana na mambo ya kijaahilia (yasiyo ya kistaarabu):

Ambae atapingana na ujahilia atahifadhi heshima yake na kuipumzisha nafsi yake, na amesalimika kusikia yanayo muudhi. Amesema -Mshindi na mtukufu-: “Samehe na amrisha mema na upinge mambo ya wajaahili” [Al-Aarafu: 199].

## Kujiepusha na kugombana na watu.

### Kusahau maudhi:

Nako ni kusahau maudhi mabaya yaliyo kupata ili uusafishe moyo wako, na wala usiudhike, Na yule mwenye kukumbuka mabaya ya ndugu zake hatokuwa na mapenzi nao, na atakae kumbuka maovu aliyofanyiwa na watu hatoishi nao Maisha mazuri, hivyo sahau -yao- uwezavyo kuyasahau.

### Kusamehe nn kufuta na kubadili baya kwa jema:

Na hii ni sababu ya kuwa na nafasi ya juu, utulivu na kuiondoa Nafsi katika kulipa kisasi.

### Ukarimu (kutoa):

Ukarimu ni sifa mzuri inayo heshimiwa na jamii, na ulivyo ubahili ni sifa mbaya yenye kuchukiwa, utoaji unaingiza upendo na kuondoa uadui, unaeleta ukumbusho mzuri na unaficha kasoro na maovu.

### Kutegemea malipo kwa Allah -mshindi na mtukufu-:

Jambo hili ni kubwa miongoni mwa yanayo saidia kupata tabia bora, kwa kuwa ni miongo mwa yanayo

saidia kuwa mvumilivu, kujipinda, na kuvumilia maudhi ya watu, pindi mwanadamu anapokuwa na yakini kwamba Allah -Mtukufu- atamlipa kwa tabia zake nzuri, na kuilazimisha nafsi yake (kuwa mwema), hakika atafanya pupa kuwa na Tabia nzuri na yatakuwa mepesi yale anayokutana nayo katika kutekeleza hilo.

## Kujiepeusha na Hasira:

Kwani hakika Hasira ni kaa la moto linalo waka kwenye moyo, linapelekea kupenda ukubwa na kutesa watu na kuepuka hasira, endapo mwanadamu ataidhibiti Nafsi yake wakati wa Hasira, hakika yeye ni mwenye anahifadhi ushindi na utukufu wa Nafsi yake, na anaiepusha na udhalili wa kuomba radhi- kwa makosa- na ubaya wa majuto. Kutoka kwa Abi Hurayrah -Allah amridhie- amesema: “Alikuja Mtu Akasema: ewe Mtume wa Allah, Niusie, Akasema: Usikasirike, Kisha akarudia mara nyingi, Akasema: Usikasirike” [Ameipokea Bukhary].

## Kukubali nasaha zenye lengo zuri, na kukosoa kwa kujenga:

Na pale anapogundua yale ambayo yana mapungufu inampasa kuifanya Nafsi yake ni yenye kuyaepuka,

kwani kuitengeneza Nafsi hakutimii bila ya kujua kasoro zake.

## Mtu kusimamia majukumu aliyopewa kikamilifu na kwa usahihi.

hili litamuepusha na kukaripiwa na kukemewa, msalimishe na udhalili wa kuomba radhi.

## Kukubali kosa linapotokea, na kuchukua tahadhari dhidi ya kulihalalisha:

Kufanya hivyo ni alama ya Tabia njema, kisha kunakusalimisha na uongo, kukubali kosa ni jambo zuri, linampandisha Mtu cheo.

## Kulazimika na ukweli:

Hakika ukweli una athari nzuri, Na kupitia ukweli kinapanda cheo cha mtu, na nafasi yake huwa juu, Ukweli unamuokoa Mtu na uchafu wa uongo na dhamira mbaya, na udhalili wa kuomba radhi, unamlinda dhidi ya kufanyiwa ubaya na watu, na kuondoka uaminifu wake, pia unampa utukufu, ushujaa na kujiamini.

## Kujiepusha na kulaumu sana na kumkaripia yule ambae amekosea:

Kwani kulaumu sana kunatia hasira, kuleta uadui, na pia ni sababu ya kusikia yanayo udhi. Na kwa mwenye akili nzuri hawezi kuwaadhibu ndugu zake kwa dogo na kubwa, isipokuwa anawachukulia Udhuru, kisha endapo kutakuwa na yanayo lazimika kukemea basi iwe kwa ulaini na upole.

## Kufatana na wema na wenye Tabia njema:

Jambo hili ni miongoni mwa mambo makubwa ambayo yanayokuza na kuithibitisha tabia njema n kwenye Nafsi ya mtu.

## Kuchunga Adabu za mazungumzo na vikao:

Miongoni Adabu zake ambazo zinapaswa kuzichunga vizuri kumsikiliza anae kuzungumzisha, na kujiepusha kukatisha mazungumzo yake, au kumuona muongo, au kumdharau, au kuondoka kabla ya kukamilisha mazungumzo yake.
Na miongoni mwazo pia, ni kusalimia pale unapoingia na unapotoka, na kupeana nafasi kwenye vikao, na wala mtu asimsimamishe mwengine na

kukaa yeye sehemu yake, na wala asiwaatenganishe waliokaa Pamoja isipokuwa kwa idhni yao, pia wasiongee kwa siri wawili bila ya kumshirikisha mwenzao wa tatu.

## Kudumisha kusoma mwenendo wa Mtume -Rehema na Amani za Allah ziwe juu yake:

Mwenendo wa Mtume inamuwekea msomaji yake mtazapo mkubwa ulioutambua ubinadamu, na uongofu na Tabia kamilifu kwenye Maisha ya kibinadamu.

## Kuangalia ki undani mienendo ya Maswaaba watukufu -Allah awaridhi.

## Kusoma vitabu vya Tabia:

kwani hivyo humzindua mwanadamu juu ya tabia njema, na vinamkumbusha ubora wake, na vinamsaidia kuzipata tabia njema, kama vile vinamkumbusha tabia mbaya, kumbainishia mwisho mbaya na njia za kuziepuka Tabia mbaya hizo.

# FIHRISI YA KITABU

UTANGULIZI ........................................................3
ALAMA ZA TABIA NZURI ..................................8
TABIA ZA MTUME -Rehema na Amani za Allah ziwe juu yake-:........................................................10
UKWELI: ........................................................13
UAMINIFU: ....................................................15
UNYEYEKEVU:...............................................16
HAYA:.............................................................17
TABIA MBAYA: ..............................................19
Dhuluma: .........................................................19
Husda: .............................................................21
Kughushi (kufanya Hadaa):..................................22
Kughurika (kujiona): .........................................23
MIONGONI MWA MBINU ZA KUPATA TABIA NJEMA: ..........................................................24
Kusalimika kwa Itikadi: .......................................24
Dua: ...............................................................25
Kupambana (na nafsi): ........................................25
Kujihisabia (kujitathmini): ..................................26
Kuzingatia matokeo mazuri ya tabia njema: .......26
Kufikiria mwisho mbaya wa tabia mbaya:..........27
Kujihadhari na kukata tamaa kwa kutotengamaa Nafsi: .............................................................27

Kujilazimisha kuwa na Bashasha na tabasamu na kujiepusha kukunja uso: ....................................27
Kusamehe na kujisahaulisha ni miongoni mwa Tabia za wakubwa na watukufu, na sifa hizi mbili ni miongoni mwa sifa zinazobakisha, na kukinga dhidi ya uadui. ....................................................28
Upole: ........................................................................28
Kupingana na mambo ya kijaahilia (yasiyo ya kistaarabu): ....................................................28
Kujiepusha na kugombana na watu. ....................29
Kusahau maudhi: ...............................................29
Kusamehe nn kufuta na kubadili baya kwa jema: ..........................................................................29
Ukarimu (kutoa): ...............................................29
Kutegemea malipo kwa Allah -mshindi na mtukufu-: .......................................................29
Kujiepeusha na Hasira:.......................................30
Kukubali nasaha zenye lengo zuri, na kukosoa kwa kujenga:...................................................30
Mtu kusimamia majukumu aliyopewa kikamilifu na kwa usahihi. ...............................................31
Kukubali kosa linapotokea, na kuchukua tahadhari dhidi ya kulihalalisha: .......................................31
Kulazimika na ukweli:........................................31
Kujiepusha na kulaumu sana na kumkaripia yule ambae amekosea:.............................................32
Kufatana na wema na wenye Tabia njema:.........32

Kuchunga Adabu za mazungumzo na vikao: ......32
Kudumisha kusoma mwenendo wa Mtume - Rehema na Amani za Allah ziwe juu yake: ........33
Kuangalia ki undani mienendo ya Maswaaba watukufu -Allah awaridhi....................................33
Kusoma vitabu vya Tabia:..................................33